# REPUBLIC OF KENYA

## COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

### THE HANSARD

**Tuesday, 7th September, 2021**

*The House met at the Assembly Chambers at 2.30 p.m.*

*[The Speaker (Hon. Patrick Waigwa) in the Chair]*

PRAYER

### PAPERS LAID

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENT BY THE TRADE, TOURISM AND COOPERATIVE COMMITTEE

**Hon. Judy Lukio:** Thank you Mr. Speaker. I beg to lay the report of Trade, Tourism and Cooperative Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly report and financial statements for the period ended 30th September, 2019 dated 7th September, 2021.

*(Hon. Judy Lukio laid the report on the table)*

LAIKIPIA COUNTY CLIMATE CHANGE BILL, 2021 PUBLIC PARTICIPATION REPORT

**Hon. Patricia Muthoni:** Thank you Mr. Speaker. I beg to lay the report of Public Participation for the Laikipia County Climate Change Bill, 2021 by the Agriculture, Environment and Natural resources Committee dated 31st August, 2021.

*(Hon. Patricia Muthoni laid the report on the table)*

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENT BY THE FINANCE AND COUNTY PLANNING COMMITTEE

**Hon. Joseph Suge**: Thank you Mr. Speaker. On behalf of the Chair, Finance and Planning Committee, Hon. Mary Samken I beg to lay a paper on report on the Committee of Finance and County Planning on the County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and the financial statement for the period ended 31st December, 2019.

*(Hon. Joseph Suge laid the report on the table)*

### NOTICES OF MOTIONS

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENT BY THE TRADE, TOURISM AND COOPERATIVE COMMITTEE

**Hon. Judy Lukio:** Thank you Mr. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

THAT, this House adopts the report of Trade, Tourism and Cooperative Committee on County Government of Laikipia (Executive) quarterly report and financial statements for the period ended 30th September, 2019 dated 7th September, 2021.

LAIKIPIA COUNTY CLIMATE CHANGE BILL, 2021 PUBLIC PARTICIPATION REPORT

**Hon. Patricia Muthoni:** Thank you Mr. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

THAT, this House adopts the report of Public Participation for the Laikipia County Climate Change Bill, 2021 by the Agriculture, Environment and Natural Resources Committee dated 31st August, 2021.

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENT BY THE FINANCE AND COUNTY PLANNING COMMITTEE

**Hon. Joseph Suge**: Thank you Mr. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

THAT, this House adopts the report on the Committee of Finance and County Planning on County Government of Laikipia (Executive) quarterly reports and the financial statement for the period ended 31st December, 2019.

**MOTION**

*[Resumption of a previous debate dated 02/09/2021]*

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS BY THE TRANSPORT AND PUBLIC WORKS COMMITTEE

THAT, this House adopts the report of the Committee on Transport and Public Works on County Government of Laikipia (County Executive) quarterly reports and financial statements for the period ended 31st December, 2019 dated 23th August, 2021.

*(Question put and agreed to)*

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS BY THE LABOUR, SOCIAL AND WELFARE SERVICES COMMITTEE

**Hon. Christopher Mark:** Thank you Mr. Speaker, Sir. On behalf of the Chair, Social, Labour and Welfare Services I beg to move the following motion;

THAT, this Assembly adopts the Report of the Committee on Labour, Social welfare and Community Services on County Government of Laikipia (County Executive) quarterly report and financial statements for the period ended 31st December, 2019 dated 26th August, 2021.

Mr. Speaker, Sir, this is a report on the period that ended on 31st December, 2019 by the Labour Committee. The Committee comprises of the following Membership;

1. Hon. Patricia Muthoni -Chair
2. Hon. Chris Mark -Vice Chair
3. Hon. Joseph Suge -Member
4. Hon. Robert Maina -Member
5. Hon. Irene Wachuka -Member

Mr. Speaker, Sir, this is a report that puts together the budget excursion by programmes and sub-programmes as you can see on page 5. It is tabled part by part and point by point to page 6 where you can see the grand totals. Mr. Speaker, Sir, I know Members have this report and for the love of information, I know they have gone through this report part by part, figure by figure and word by word. Mr. Speaker, Sir, if you go to page 7 on the committee observations;

1. There is an increase in the compensation of the employee vote. This vote encompasses the basic salaries of permanent employees. Basic wages of temporary

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

employees, personal allowances paid as part of salary and pension and other social security contributions.

2. The policy development vote and the fire services votes have not been utilised.
3. The children support program had an increased absorption rate. This expenditure relates to the school fees that was paid for the students of the Laikipia Rescue and Rehabilitation Centre.

On the Committee recommendations;

1. The department should ensure that optimal staffing levels are maintained so as to keep the current wage bill at manageable levels.
2. The department may formulate policies to guide operations within the department and the county as a whole.
3. The department should ensure that the child support programme vote has been utilised so as to cater for the children's basic needs.

Mr. Speaker, Sir, the conclusion is that this House adopts the committee's report on County Government of Laikipia (County Executive) Quarterly report and financial statements for the period ended 31st December, 2019.

Mr. Speaker, as a Committee on Labour we are passionate when we are talking about the issues of wage bill. As you all know the oversight of the public service of this county falls under this committee. When the wage bill is rising to a point that it competes or supersedes development, it will leave a lot of questions because the Financial Act and the PFM has a clear indication that it should not bypass 36% to 40%.

Currently, we are doing beyond that. With these few remarks I would urge Hon. Members to support this and make their contributions on it. With that said, I will call upon the able Chair, Labour, Social Welfare and Community Services Committee to second. Thank you.

**Hon. Patricia Muthoni:** Thank you, Mr. Speaker. I rise to second this motion and I ask Hon. Members to support this motion. I second.

*(Question Proposed)*

**Hon. Stephen Ndiritu:** Asante, Bwana Spika. Nasimama kuunga mkono ripoti ya Kamati ya Utendakazi. Hii ni ripoti ambayo inaeleza jinsi Idara imekuwa ikitumia pesa katika sekta zake. Nikiangalia hii ripoti na vile kamati imeweza kueleza inaonyesha Idara zingine zinahitaji kumulikwa zaidi kwa sababu ni lazima kazi ambayo inahusu mwananchi iweze kufanyika.

Nasema hivi kwa sababu nimekuwa mmoja wa hiyo kamati kama mwanakamati hata kama sijui kulienda aje nikajikuta nje. Huwa nashukuru kwa uhai na bado naunga mkono kazi nzuri ambayo inafanywa na kamati hata kama mimi si mwanakamati. Bwana Spika, nimeona kile ambacho kamati iliangalia. Huwa nasema mara mingi kwamba kamati ambayo iko na ripoti katika Bunge hili hufanya hivyo kwa niaba ya Bunge.

Kwa hivyo kama kuna mahali kuna shida sisi kama Bunge ndio tutarekebisha. Kwa mfano katika hii idara waliweza kupewa pesa lakini pesa hazikuweza kutumika hasa upande wa kuzima moto na mambo mengine ya dharura. Hiyo idara ilichelewa na haikuweza kutumia hizo pesa kwa njia ambayo inafaa ilhali tunajua ni ngumu sana Laikipia ipite miezi tatu ama nne bila kupata janga la moto.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kusikia kuna pesa ambazo hazikutumika tuko na tashwishi na tunajiuliza pesa ambazo tunaweka hapo zinafanya kazi. Hilo ni jambo sisi kama Bunge na kama vile kamati wameweza kueleza hapa tutafuatilia. Kama hakukuwa na shida, inshallah na tunashukuru lakini kama kulikuwa na shida tutaangalia na tuone kama kuna watu wamelegea kwa hiyo kazi. Naunga kamati mkono na hii ripoti ni kama taarifa ya benki ambayo huwa inatoka. Kama imetoka ni vizuri kuangalia kama kuna mahali kuna makosa.

Hii ni kama taarifa ya benki ambayo hutoka, na itokapo ni vizuri kuiangalia kuona iwapo ina makosa. Mara nyingi inakueleza kinagaubaga kwa sababu ni kitu ambacho huwezi badilisha. Kama wamesema hawakutumia pesa basi hawakutumia, kwa sababu inaonyesha kuwa hawakutumia. Kama wametumia ni lazima ionyeshe wametumia vipi. Ninayotaka kuzingatia hapa ni kwa nini pesa ambayo tunapitisha katika hili Bunge haitumiki?

Nashukuru kwa sababu mpango wa usaidizi kwa watoto ulitumia pesa hata zaidi. Hilo ni jambo ambalo linakubalika kwa sababu wale watoto ambao husaidiwa, tukiweza kuwasaidia hata zaidi kuliko tulivyowasaidia litakuwa ni jambo la busara. Katika sehemu hiyo naona kuwa walifanya vizuri kwa sababu wale watoto mara nyingi hutegemea serikali na wafadhili.

Bwana Spika, kuna mambo yanayozungumziwa hapa kuhusu mishahara. Mishahara ya wafanyakazi ni jambo ambalo limetatiza hii Kaunti kwa sababu pesa nyingi, kama wakati huu ambapo tumefanya bajeti, tumepata kwamba zaidi ya bilioni tatu inaelekezwa upande wa mishahara. Hilo ni jambo linalofaa kuangaliwa na nafikiri kamati itafanya uchunguzi na kuita wahusika wote, hata Bodi ya *Public Service Board*, waweze kueleza kile wanachofanya kuhakikisha kwamba kiwango kikubwa cha pesa ya Wanalaikipia haitumiki katika mishahara.

Tungetaka kuona ya kwamba asilimia kubwa ya pesa inatumika katika maendeleo. Ikienda kinyume na hiyo inaonyesha kwamba Kaunti yetu ya Laikipia haitaweza kupata maendeleo. Hilo ni jambo ambalo ningetaka kamati ifuatilie na kuhakikisha ya kwamba wametumia ujuzi wao na mbinu zote hizo pesa zisitumike.

Kwa upande wa vibarua wanaoajiriwa, yeyote anayeajiriwa, awe kibarua, mfanyakazi wa kudumu au mkandarasi, mwisho wa siku analipwa na pesa ya Mwanalaikipia. Kwa hivyo hilo ni jambo tunalofaa kukaa na kuliangalia. Hatusemi watu wasipewe kazi, ni lazima kazi ifanyike. Lakini tujiulize iwapo kazi zinazofanywa zinaleta manufaa kwa Wanalaikipia. Mfano mzuri ni watu ambao wamepewa kazi, nami ningetaka Kamati ya Uchukuzi na Kazi za Umma iangalie, kuna watu waliopewa kandarasi hasa kwenye upande wa mashine za kukodisha. Unapata kwamba huyo mtu anasemekana kuwa anafanya kazi ilhali hajawahi kuingia kazini mwezi mmoja au miwili.

Hilo ni jambo tunalofaa kuangalia kwa sababu utapata kuwa pesa ya serikali mara nyingi hupotelea hapo. Pia kuna Idara ya Kilimo na Mazingira, huko pia kuna shida. Kamati zilizo kwenye hili Bunge zinastahili kufanya uangalizi na kuhakikisha kuwa hakuna ubadhilifu wa pesa za Laikipia. Naongea kuhusu utumizi wa pesa kama Mwenyekiti wa Bajeti ambaye anataka kuhakikisha ya kwamba pesa iliyotengewa sekta yoyote inatumika kwa njia ifaayo.

Ni lazima pia tuelewe wale tunaoambiwa wameongezewa pesa za marupurupu, ni marupurupu gani? Naona mambo ya pesa za kustaafu bado yako hapa. Ni lazima tuchunge pesa. Juzi nilisema kwamba tutachunga pesa ya Laikipia kama maziwa jikoni. Ningeomba wote walio kwenye hili Bunge pamoja na kamati zinazofanya uangalizi wawe makini na waangalie. Kazi ya Kamati ya Bajeti ni kuhakikisha kuwa tumezipa hizo idara pesa ya kutosha.

Tukishapeana hizo pesa, kuna Kamati ya Fedha na ya Leba inayoongozwa na Mheshimiwa Patricia ambayo inatueleza kinagaubaga na kuangalia jinsi ambavyo pesa

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

inatumika. Kuna Kamati ya Utekelezaji ambayo ni ya Mheshimiwa Suge, atuambie ni kamati gani inayofanya kazi na ni kazi gani ambazo zinafanyika. Wakati huu ni kama wengi wetu tumejiunga na mambo ya siasa na kusahau kutekeleza miradi. Wengine wameingia kwenye rukwama na wengine sijui chama gani, kila mtu ana chama.

La muhimu tukifika kwenye Bunge hili sio mambo ya rukwama. Huyu Mheshimiwa Suge aache kutuambia mambo ya rukwama, atuambie jinsi ambavyo utekelezaji unatendeka katika Laikipia yetu. Hayo ndiyo mambo tunayotaka yazingatiwe na kupewa kipaumbele kwa sababu ifikapo mwisho wa siku tunataka faida ya pesa na wananchi wetu wafanyiwe kazi. Ninaunga mkono na kukubaliana na hii ripoti, ahsante.

**Hon. Joseph Suge:** Asante sana, Mheshimiwa Spika. Ningependa kutoa maoni yangu kuhusu hii ripoti iliyowasilishwa na Kamati ya Leba. Nimepitia ripoti na kuona kamati wamefanya kazi kadri ya uwezo wao. Ripoti iliyowasilishwa na idara ya maswala ya wafanyakazi ni ripoti nzuri. Kabla ya kutoa mchango wangu, nataka nimjibu mwenzangu kwamba hili ni Bunge ambalo viongozi waliomo wamefika kupitia vyama mbalimbali.

Mimi kama mwakilishi wa watu wa Rumuruti nilifika hapa kupitia tiketi ya Chama cha Jubilee na bado niko kwenye hicho chama. Kwa hivyo taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa kutoka Thingithu ni porojo na mambo yasiyokuwa na maana. Safari ifikapo ukingoni kila mtu atajua atakapopitia. Nikiangalia hii ripoti...

**Hon. Stephen Nderitu:** Bwana Spika, ningetaka ufafanuzi zaidi kutoka kwa Mheshimiwa Suge ambaye amesema yeye ni wa Jubilee na yeye si wa Chama ya toroli. Ningetaka asimame katika Bunge hili aseme na akiri ya kwamba, yeye hayuko kwa chama ya toroli kwa sababu mara si haba tumemuona katika ile chama.

**Speaker:** Hon. Suge…..

**Hon. Joseph Suge:** Mheshimiwa Spika, unajua wakati mwingine mimi kama Kiongozi ambaye nina uzoefu wa miaka mingi, ninapigwa na butwaa ama mshangao ninaposikia mmoja wa viongozi akitaja toroli. Hakuna chama ambaye inaitwa toroli, chama ambaye ninajua ni chama cha UDA, ambaye alama yake ni toroli. Nafikiri Mheshimiwa ameelewa vizuri, sisi wakati tunafanya kazi….

**Speaker:** Hon. Christopher Mark

**Hon. Christopher Mark:** Mr. Speaker, Sir. Maybe a bit of clarification because am worried when Hon. Suge he says that the party he knows is UDA for wheelbarrow. How does he know this party? You know this is the party that I recognise; this is the party that I am a member and this business should be inquired. Just a clarification, you know he is my Whip and I do not want him to whip me to the wheelbarrow side…

**Speaker:** Hon. Suge…..

**Hon. Joseph Suge:** Asante, Mheshimiwa Spika. Vyama vingi kwa wakati huu wanaendelea kusajili wanachama na ilhali Mheshimiwa Christopher Mark akisimama kunielekeza kwa chama kingine ni vizuri awe na uhakikisho ya kwamba nimejisajili katika chama gani. Kwa sasa hivi mimi ni mwanachama sugu wa Jubilee na kwa hivyo hii ni taarifa tu haina mwelekeo.

Ningeomba ikiwezekana wakati mmoja unaweza kutupeleka mahali tuweze kupitia mafunzo kidogo na kuweza kuelewa chama ni nini na chama kinasaidia wanasiasa kwa njia gani ndio kila mmoja aweze kuelewa. Tunaweza kuwa hapa mwingine afikirie unaweza kuwa kwa vyama vitatu ama nne.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kwa sababu nimetoka hapo nirudi sasa kwa taarifa kamili kuhusiana na ripoti, nimeangalia kulingana na hii ripoti fedha ambaye iliweza kutumika na ile ambaye ilikuwa imetengwa. Wengi wameongea juu ya mishahara ambaye imepanda ikilinganishwa na ile fedha ambaye inatengwa kwa ajili ya maendeleo ya wanalaikipia.

Hio inanikumbusha miaka mawili ambapo Bunge hili iliweza kusimama kwa kauli moja na kupitisha mswada ambaye ilikuwa inaangazia kupunguza fedha matumizi kwa ajili ya wale wafanyikazi. Ilifika mahali ambapo watu walitolewa wengine wakafurushwa na wengine wakatolewa na mpaka saa hii na wengine wanadai pesa zao na wengine wameshalipwa.

Swali ambaye tunastahili kujiuliza ni kwamba baada ya wale ambao walitolewa, kama hizo pesa ziliweza kurudi chini. Tunapoongea, Kaunti yetu ya Laikipia sasa asilimia hamsini na sita inaenda kwa malimbikizo ya mishahara, ambaye imepita kiwango kwa sababu wanalaikipia wangestahili wapate asilimia sabini kwa maswala ya maendeleo. Nimeangalia pia katika matumizi nikaona idara imejaribu kutumia. Nirudi tu kwa maswala ambaye inahusu michezo naona kuna pesa ilikuwa imetengwa, na iliweza kutumika zote kwa sababu Kaunti yetu imekuwa ikiwasaidia wafanyikazi katika maswala ya michezo.

Ningeomba Bunge hili tunapoangalia kusonga mbele, tuangalie pia vile tunaweza saidia vijana kule mashinani wanaofanya mazoezi na wanaokuwa na taaluma mbalimbali waweze pia kusaidiwa na ili talanta zao ziweze kukuzwa katika kaunti yetu.

Tungependa miaka ingine ijayo nchi na taifa inavyowakilishwa katika michezo za dunia, Laikipia pia kuwe na vijana ambao wamejikakamua kuwakilisha taifa katika hiyo michezo. Nimeangalia mambo ya fidia kwa wafanyikazi na ninajua kwamba hii ni kuhusiana na wale pengine wengine wanastaafu, na wengine wamefanya kazi waweze kupata pesa zao.

Ni vizuri kama kamati watafuatilia kuona yule mtu ambaye amefanya kazi, kama ni yule daktari ambaye ametoa mgonjwa kutoka Nanyuki hadi Nairobi ama kutoka Nanyuki hadi Meru, anaweza kulipwa zile pesa zake ya ile masaa iwapo ni ya usiku. Mchana pia wanaweza kupata kwa wakati mzuri kwa sababu wakati mwingine watu wanazembea kazini kwa sababu ya kutoangaliwa kwa mambo kama yale..

Nikiangalia *disaster reduction management,* naona pia kuna pesa ambazo zilitengwa na ziliweza kutumika kiasi fulani. Ningeomba kwa bajeti ambayo itakuja, hii pesa ya *reduction* kwa sababu sasa tuna sheria ambayo inazingatia matumizi ya hizi pesa, iweze kuongezwa.

Maswala ya mambo ya moto, sehemu nyingi zimeadhirika kwa sababu ya maswala ya moto na wakati mwingine watu wanastahili kusaidiwa kwa sababu nyumba inaweza kuchomeka na kila kitu kichomeke na watu wakose malazi. Kwa hivyo hizo pesa zinafaa kuangaliwa na kupewa kipao mbele. Kwa hayo machache ninaunga mkono na kuwashukuru wana kamati, asante.

**Speaker:** Who was the mover? Hon. Chris, kindly do reply.

**Hon. Chris Mark:** Thank you, Mr. Speaker. I would like to thank all the colleagues who have made their contributions and even the serious pointers that have come from them concerning the utilization especially of the funds for fire. I don't know whether it is because we have never had a disaster management bill and the Chair is here with the committee and we need to pressure for that to be assented to. I don't think that it has ever been assented into law. Maybe there were restrictions on how those funds could be used but now there is a framework, it is very important they are utilized because we do not pray for disasters but we all know that we are prone to disasters now and then especially like what is happening in Olmoran area.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Issues on monies and the rising wage bill that is a conversation that is even beyond the committee. We should have the conversation both as County Executive and the Assembly to see how we can tame the rising wage bill. I thank all the Members who have supported in contribution and some in silence. Someone like Zamzam made me know that she was overwhelmed with such a good report. She did not know what to do and therefore supported in silence. So I call the Members to vote on it. Thank you.

*(Question put and agreed to)*

## COMMUNICATION FROM THE CHAIR

PLACEMENT OF THE NEW MEMBER IN COMMITTEES

**Speaker:** Maybe before we finish, the Chairperson for Selection Committee who is also the Majority Leader, we have a new Member by the name Hon. Lochimidi. I believe that I directed last week that we need to place him in some committees. I believe that it will be against his rights if he continues to be in this House yet he cannot serve in any committee and the committees continues to meet. I believe that from his maiden speech which he made in this House, he is very enthusiastic and also willing to participate in business.

Therefore, let the Selection Committee move with speed and ensure that we place that Member in a number of committees because he deserves to be in a number of them. Therefore, I wish that we do that by the end of this week on Thursday. Let the committee meet and allocate him some committees because it is important. He has come to this House late and therefore it is important that he also moves with speed so that he can be able to deliver to the people he represents, that which he is willing to.

## ADJOURNMENT

**Speaker:** This House stands adjourned until tomorrow Wednesday, 8th September, 2021 at 9.00 a.m.

The House rose at 3.04 p.m.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*